**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**KWA MWAKA 2023/2024**
**ILIYOSOMWA NA**

**MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME (MBM)**
**WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

**JUNI, 2023**



**MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME (MBM)**
**WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

## YALIYOMO

UTANGULIZI ..... 1
UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ..... 2
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023 ..... 5
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023 ..... 6
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ..... 7
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ..... 14
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ..... 14
Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ..... 15
Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) ..... 16
Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC). . 18
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI ..... 20
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini ..... 21
Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini ..... 23
Kampuni ya Uvuvi Zanzibar – ZAFICO ..... 24
Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari ..... 25
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ..... 26
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji ..... 27
Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ..... 28
Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba ..... 29
CHANAGAMOTO ..... 30
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDH 2023/2024 . 31
MAKADIRIO YA MAPATO 2023/2024 ..... 31
MAKADIRIO YA MATUMIZI 2023/2024 ..... 31
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA ..... 32
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ..... 32

MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2023/2024 ........ 35
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU .......... 37
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ........ 38
Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) ........ 39
Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, ZPDC ... 40
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI ........ 41
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini ........ 42
Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini ........ 43
Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ........ 44
Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari ........ 45
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ........ 46
Programu Ndogo ya utawala na uendeshaji ........ 46
Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ........ 47
Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba ........ 48
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024. ........ 49
HITIMISHO ........ 50
VIAMBATANISHO ........ 53

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Kazi za Kawaida na Kazi za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambayo yanawasilishwa katika Mfumo wa Programu (PBB).

2. **Mheshimiwa Spika,** Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki kinachojadili Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

3. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa anaoutoa kwenye Maendeleo ya Nchi yetu. Shukurani za pekee zimuendee Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, mashirikiano, usalama, amani na utulivu. Hatua hiyo imepelekea utekelezaji mzuri wa malengo ya Serikali katika kuleta Maendeleo ya Sekta za Uchumi wa Buluu na Uvuvi na hatimae kukuza Uchumi wa Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kumshauri vizuri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufikia azma yake ya kuboresha uchumi na maisha ya Wazanzibari. Vile vile, shukurani za pekee

ziende kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwashauri vyema viongozi wetu na kufanya maamuzi yenye hekima na busara katika kuleta Maendeleo ya Zanzibar.

5. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii adhimu kwa dhati kabisa kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi. Pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayoifanya na tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

6. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kwa namna ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, pamoja na Wajumbe wote na Sekretarieti ya Kamati hiyo, kwa miongozo na ushauri waliyotoa kwa Wizara katika kufanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2022/2023, na kuendelea kutusaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Napenda kuihakikishia Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo mliyoyatoa yamezingatiwa katika ukamilishaji wa bajeti hii kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.

## UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

7. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, inaendeleza kazi ya kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kiuchumi kupitia sekta ya Uchumi wa Buluu.

8. **Mheshimiwa Spika,** Lengo Kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kuimarisha matumizi endelevu ya bahari na kuwawezesha Wajasiriamali kwa kuwapatia elimu, uelewa na ufahamu zaidi, ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana

za ujasiriamali, uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya Uvuvi, Mazao ya baharini, Mwani, Biashara za baharini, Utalii, Mafuta na Gesi Asilia na Nishati mbadala.

9. **Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa lengo hilo, mkazo zaidi utawekwa kwenye maendeleo ya viwanda vya kusarifu samaki, mwani na mazao mengine ya bahari ikiwemo mitambo ya kuhifadhia samaki, madiko na masoko ya minada na ujenzi wa bandari jumuishi za uvuvi. Malengo yote haya yatasaidia katika kufikia shabaha zote zilizooanishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 ikiwa pia upatikanaji wa ajira kwa vijana kupitia Uchumi wa Buluu.

10. **Mheshimiwa Spika,** Uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka **tani 47,111** mwaka 2021 hadi **tani 61,794** kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 31**. Uzalishaji wa samaki kwa mwaka 2021 ulikuwa na thamani ya **Shilingi 237,148,468,042** kulinganisha na uzalishaji wa samaki kwa mwaka 2022 wenye thamani ya **Shilingi 391,370,146,212**. Kwa mwaka 2022 wastani wa thamani ya samaki kwa kilo moja ilikuwa ni **Shilingi 6,333**. Mchango wa Sekta ya uvuvi kwa thamani ya pato la Taifa umeongezeka kutoka **Shilingi 236.8 Bilioni** kwa mwaka 2021 hadi kufikia **Shilingi 243.0 Bilioni** kwa mwaka 2022. (**Kiambatanisho Namb. 1A)**.

11. **Mheshimiwa Spika,** Usafirishaji wa mazao ya baharini ikiwemo matango bahari, mwani, dagaa, kaa na pweza umeongezeka kutoka **tani 19,063** mwaka 2021 hadi **tani 23,158** mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 21 (Kiambatanisho Namb. 1B)**. Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka **tani 10,531** mwaka 2021 hadi **tani 12,594** kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 20**. Usafirishaji wa mwani nje ya Nchi umeongezeka kutoka **tani 12,124** mwaka 2021 hadi **tani 13,972** mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 15**.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Uvuvi wa bahari Kuu, hadi kufikia Aprili 2023, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority - DSFA) ilikuwa imetoa leseni za uvuvi wa bahari kuu 48, kati ya hizo, leseni tatu zilikuwa ni kwa meli za ndani na leseni 45 zilitolewa kwa meli za uvuvi za nje, na vibali vya kuvua nje ya mipaka ya ukanda wa uchumi wa bahari ya Tanzania (Areas Beyond National Jurisdiction) kwa meli saidizi (supply vessels) tano (5) pia vilitolewa. Kwa ujumla Mamlaka iliweza kukusanya jumla ya Shilingi za Kitanzania **Bilioni 6.2** (sawa na asilimia 115 ya makadirio ya kukusanya **Shilingi Bilioni 5.4** kwa mwaka) ikilinganishwa na leseni 25 zilizotolewa katika kipindi kilichopita na zilizokusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 3.3**. Kuimarika kwa makusanyo yatokanayo na leseni za uvuvi wa bahari kuu kunatokana na juhudi za makusudi zilizofanywa na viongozi wetu wakuu wa kitaifa ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira rafiki ya kuvutia uwekezaji yaliyopo katika Sheria ya Uendelezaji na Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388 ya mwaka 2020, Kanuni zake za mwaka 2021, Sera na Vivutio vya Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na Mpango Mkuu wa Uvuvi wa Jodari katika Bahari Kuu.

13. **Mheshimiwa Spika**, Katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, mafanikio makubwa yamepatikana baada ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukabidhiwa Data za Mafuta na Gesi Asilia kutoka Wizara ya Nishati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Data hizo za Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Pemba – Zanzibar na vitalu Nam 9 mpaka 12, zilikuwa zikihifadhiwa kwa muda mrefu kisheria huko Tanzania Bara. Data hizo zitasaidia kuyagawa upya maeneo yenye mwelekeo wa Mafuta na Gesi Asilia katika vitalu hivyo upya na baadae Zanzibar itaweza kuingia mikataba na makampuni makubwa kwa ajili ya uekezaji katika maeneo hayo.

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa hivi sasa Wizara imeingia mkataba na Kampuni ya Schlumberger kutoka Ufaransa kwa kazi ya Uchambuzi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia kwa lengo la kufungua maeneo mapya ya uwekezaji katika sekta ya Mafuta

na Gesi Asilia katika maeneo ya Mashariki ya bahari ya visiwa vya Zanzibar, na kwamba tayari kampuni hiyo imeanza kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mkataba ambapo kazi hizo zimepangwa kukamilika baadae mwaka huu.

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023

15. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesimamia utekelezaji wa Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, Mpango wa Maendeleo Zanzibar kwa mwaka 2021 – 2026 (ZADEP), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), pamoja na Sera na Mipango Mikakati ya Kisekta ya Uchumi wa Buluu, ikiwemo ya uvuvi na Mafuta na Gesi Asilia. Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wavuvi, wakulima wa mwani, na wafugaji wa mazao ya baharini. Aidha, mikakati hiyo imesaidia kujenga uelewa kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi kuhusu uwekezaji na uwezeshaji katika sekta ya Uvuvi, Mwani, ufugaji wa viumbe maji, Mazao ya Baharini, Utafiti, uhifadhi wa maeneo ya bahari, na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

16. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imetekeleza malengo yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni:

    i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu
    ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi
    iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

17. **Mheshimiwa Spika**, Kupitia Programu hizo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutekeleza jumla ya Miradi tisa (9) **(Kiambatanisho Namb. 2)**.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 2,259,412,000** kupitia vianzio vyake vinne vya Unguja na Pemba, ikiwa ni pamoja na Ada za uvuvi, Ada ya mazao ya baharini, Mapato ya uvuvi wa Bahari kuu na Ada ya uingiaji wa wageni katika hifadhi za maeneo ya bahari. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 2,738,332,412** sawa na **asilimia 155** ya makadirio ya miezi tisa **(Kiambatanisho Namb. 3)**.

19. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 89,662,400,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,107,400,000** zilikuwa ni kwa kazi za kawaida na **Shilingi 81,555,000,000** zilikuwa kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Mgawanyiko wa fedha kwa kazi za kawaida ni **Shilingi 8,107,400,000**; Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,429,800,000** Mishahara, **Shilingi 3,269,800,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 2,407,800,000** ni Ruzuku kutoka SMZ. Aidha, kwa fedha za Ruzuku, **Shilingi 320,000,000** ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini (ZAFIRI), **Shilingi 1,775,300,000** ni kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na **Shilingi 312,500,000** ni kwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO). Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliidhinishiwa **Shilingi 81,555,000,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 52,000,000,000** kutoka SMZ na **Shilingi 29,555,000,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

20. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2023, Wizara imepata jumla ya **Shilingi 22,043,016,785** sawa na **asilimia 25** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,977,609,476** ni kwa kazi za kawaida, ambapo **Shilingi 2,573,276,583** ni Mishahara, **Shilingi 700,762,832** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, na **Shilingi 1,703,570,061**

ni Ruzuku kutoka SMZ **(Kiambatanisho Namb. 4**). Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara imeingiziwa jumla ya **Shilingi 17,065,407,309**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,070,000,000** kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na **Shilingi 14,995,407,309** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo **Shilingi 11,599,214,123** ni kutoka JICA kwa mchango wa ujenzi wa Diko na Soko la kisasa Malindi ambao umekamilika. **Shilingi 3,016,019,434** kutoka Benki ya Dunia kwa mradi wa SWIOFISH ambao nao tayari umekamilika na **Shilingi 380,173,752** kutoka shirika la IFAD kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya kilimo na Uvuvi ambao bado unaendelea. **(Kiambatanisho Namb. 4).**

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**21. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2022/2023, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilitekeleza programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:

i. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeipatia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi jumla ya **Shilingi Bilioni 36.5** kutoka katika mfuko wa Fedha za Ahueni ya UVIKO19 za IMF. Kupitia programu hiyo, Mafanikio makubwa yanaendelea kupatikana kama ifuatavyo:

- Jumla ya **boti 827** tayari zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 14** zimetengenezwa na zimeanza kugawiwa kwa wananchi. Kati ya boti hizo, **boti 500** ni za mita 5 kwa ajili ya wakulima wa mwani, **boti 250** za mita 7 kwa ajili ya wavuvi wanaotumia mishipi na **boti 98** za mita 8 kwa ajili ya uvuvi wa nyavu.

- Jumla ya **boti 314** (Unguja 98 Pemba 216) tayari zimetolewa kwa wananchi 3,140. Kati ya hizo, **boti 112** ni kwa wakulima wa mwani 1,120 na boti zilizobaki 202 zilitolewa kwa wavuvi 2,020.

- Wizara imechangia **Shilingi Bilioni 2.5** katika ujenzi wa Kiwanda cha mwani Chamanangwe Pemba. Kazi inaendelea kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

- Wizara, kupitia Kampuni ya ZAFICO, tayari ipo katika mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa huko Kama ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa chanja maalum za kuanikia dagaa bora na litakalokuwa na bei ya ushindani katika masoko ya kimataifa. Tayari ZAFICO imejenga kituo cha ugani cha kuelemisha njia bora na za kisasa za uchemshaji, ukaushaji, uhifadhi, usindikaji na utayarishaji wa bidhaa za madagaa. Aidha, katika hatua za awali jumla wajasiriamali 90 wamepatiwa mafunzo ya uanikaji dagaa.
- Wizara pia kupitia Mradi huu wa Ahweni ya UVIKO19 imenunua vifaa vya ukulima wa mwani kama kamba na taitai vyenye thamani ya **Shilingi 1,750,000,000** kwa ajili ya wakulima 5,000 wa mwani ambao wengi wao na kwa asilimia kubwa kabisa ni akina mama. Vifaa hivi vilikabidhiwa kwa Kampuni ya Serikali ya mwani kwa usambazaji kwa wakulima hao.
- Ununuzi wa mtambo wa kutengenezea chakula cha samaki wenye thamani ya **Shilingi 139,000,000** umekamilika na kwa mtambo huo tayari kufika nchini kuelekea kwenye mchakato wa ujenzi na uzalishaji.
- Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa mashamba 61 ya ufugaji wa matango bahari yenye thamani ya **Shilingi Milioni 247**, mashamba 30 ya ufugaji wa Kaa yenye thamani ya **Shilingi Milioni 114.9** na mabwawa 20 ya Ufugaji wa Samaki yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1.07.** Mashamba hayo yamewanufaisha wastani wa wananchi 1,111.
- Mafunzo kwa wajasiriamali wa sekta ya uvuvi, wafugaji wa mazao ya baharini na wakulima wa mwani yametolewa, ambapo jumla ya wajasiriamali 4,000 wamepatiwa mafunzo hayo. Aidha, mafunzo maalum ya matumizi ya vifaa vya “GPS” na “Fish Finder” yamefanyika kwa walimu 70 na wavuvi 200 Unguja na Pemba.

- Wizara kwa kushirikiana na Benki ya CRDB imetayarisha mpango maalum wa utekelezaji wa huduma za mikopo ya maboti au "Business model" ikiwa ni dira ya utekelezaji wa programu ya Ahueni ya Uviko 19. **(Kiambatanisho Namb. 5)**

ii. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imekamilisha kuweka misingi ya Sera na Sheria za sekta za Uchumi wa Buluu kama vile:

- Kukamilishwa kwa Sera na Mpango Mkakati wa Uchumi wa Buluu sambamba na kukamilika kwa Sera na Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini.

- Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekamilisha Mpango Mkuu wa Uvuvi (Fisheries Masterplan), Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan); na Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Mwongozo wa Hiari wa FAO wa Kuhakikisha Uvuvi Endelevu Mdogo Mdogo (National Plan of Action on FAO Voluntary Guidelines on Small Scale Fisheries);

- Wizara pia, imekamilisha na inaendelea kutekeleza Mkakati wa Utekelezaji wa Ukondoishaji Masuala ya Kijinsia katika Uchumi wa Buluu (Gender Action Plan on Blue Economy). Pia, Wizara imekuwa katika hatua ya mwisho ya uwasilishaji Serikalini wa Rasimu za Sheria za Uvuvi, Sheria ya Uhifadhi wa Bahari na Sheria ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

iii. Wizara imekamilisha Ujenzi na Ufunguzi wa Diko na Soko la Kisasa la Samaki Malindi lenye uwezo wa kuhudumia wananchi 6,500 kwa siku, kuweka mitambo ya baridi yenye uwezo wa tani zinazofikia 200 kwa wakati mmoja na kuweka mtambo wa kuzalishia Barafu. Soko na Diko hilo litatoa mchango mkubwa katika kuendeleza biashara na huduma muhimu kwa wavuvi na wananchi kwa Ujumla.

iv. Jumla ya Miradi 17 yenye thamani ya wastani wa Dola za Kimarekani **Milioni 135** imeandaliwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Washirika wa maendeleo mbali mbali na inategemewa kuanza kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024.

v. Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imeingia ubia katika mfumo wa (Public-Private Partnership) na Kampuni ya &Beyond katika usimamizi wa eneo maalum (Marine Special Area) lililopo karibu na Kisiwa cha Mnemba. Hatua hiyo itaongeza Usimamizi wa Rasilimali na kiwango cha mapato ya jamii na Serikali kwa zaidi ya asilimia 100%.

vi. Wizara kupitia taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini (ZAFIRI) imeingia makubaliano na Kampuni ya Afrivision katika uendeshaji wa kituo cha kutotolea vifaranga vya Samaki, Kaa na Matango Bahari na kuanzishwa kwa Kampuni ya Zanzibar Marine Hatchery Limited. Aidha, uzalishaji wa matango bahari umeanza katika hatua za awali ambapo wastani wa matango bahari wachanga (Fingerling) Milioni mbili na laki tatu vimezalishwa. Kazi inayoendelea ni kuvilea katika kipindi hichi cha mpito kwa vimalea kuendelea kukua bila ya athari zozote zile za kimaumbile hadi kufikia hatua ya kukabidhiwa wananchi katika utaratibu maalumu.

vii. Wizara imeingia Hati ya makubaliano na kampuni ya Evergreen Egypt United, kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu, kuanzisha viwanda vya kusarifu samaki pia kufanya ufugaji wa mazao ya Baharini Zanzibar. Wizara imesaini hati ya mashirikiano na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) kupitia Kampuni ya Chemonics International ambayo inatekeleza Mradi mpya wa Uchumi wa Buluu wa ”Heshimu Bahari”. Halikadhalika, upitia kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) Wizara imesaini hati za makubaliano na Kampuni ya ZANZIFRESH yenye wadau

kutoka Marekani pamoja na Senegal kwa madhumuni ya kuleta meli za uvuvi wa Bahari Kuu na kujenga Mitambo ya Baridi na Kuchakata samaki.

- ZAFICO kuingia katika Hati za Makubaliano na Kampuni za APPLE TREE ya KOREA kwa ajili ya Ufugaji wa kamba na Kuanzisha mitambo ya baridi yenye kutumia nishati ya jua. Miradi ya Kampuni hii ya Apple Tree inafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) na Shirika la Nishati la Korea (Korea Energy Agency)

viii. Wizara kupitia Mradi wa SWIOFISH imekamilisha kazi ya uwekaji maboya 33 kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya maeneo ya uhifadhi wa bahari pamoja na uhifadhi wa maeneo muhimu ya mazalia ya samaki kwa uvuvi endelevu

ix. Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania (DSFA) imetoa mafunzo ya Waangalizi wa Uvuvi (Fishery Observers) wa bahari kuu kwa watumishi wa umma kumi (10) . Mafunzo hayo yaliyotolewa na Taasisi ya "CapMarine" ya Afrika Kusini na kufanya idadi ya Waangalizi kufikia 17. Ongezeko hilo la idadi ya Waangalizi wa Uvuvi litaongeza ufanisi wa DSFA katika kusimamia kikamilifu shughuli za uvuvi wa bahari kuu.

x. Kazi ya matayarisho ya Mpango Mahsusi wa Matumizi ya maeneo ya Bahari (Marine Spatial Planning) inaendelea ambapo Tathmini ya awali "Scoping & Pre-Feasibility study" ya Mpango wa Matumizi ya Bahari kwa Tanzania imetayarishwa na kuwasilishwa kwa wadau wote nchini. Tathmini hiyo imefanywa kupitia Shirika la TNC, Ofisi ya Makamo wa Rais SMT na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu hii imefadhiliwa na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kupitia Mradi wa IKI-BMU.

xi. Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini, katika kushajihisha ujasiriamali wa fursa za

Uchumi wa Buluu katika ufugaji wa viumbe maji, imeandaa Kitabu cha Muongozo wa Kitaalamu wa Ufugaji wa Matango Bahari Weupe . Muongozo huo utagawiwa kwa wafugaji wa matango bahari bila ya malipo.

xii. Uzinduzi wa mradi wa uwezeshaji wa wanawake vijijini unaofadhiliwa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa “Rural Women Economy Empowerment Project” wenye thamani ya dola za Kimarekani Milioni 5 kwa Tanzania ulikamilika mwaka jana. Mradi huu unatekelezwa katika Mikoa ya Singida, Dodoma na Mkoa wa Kusini Unguja. Kwa upande wa Zanzibar, Mradi huu utatekelezwa Wilaya ya Kusini Unguja na unahusiana na uzalishaji wa zao la mwani, na tayari matayarisho ya Mradi huu yanaendelea kupitia wadau wa maendeleo

xiii. Wizara pia inaendelea na kushirikiana utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo inayofadhiliwa kupitia mifuko mbali mbali kama vile Mradi wa “Bahari ni Mali” unaofadhiliwa na Serikali ya Ireland. Miradi mengine miwili inayofadhiliwa kupitia Mfuko wa Blue Action Fund ipo tayari kwa utekelezaji. Miradi hiyo ni pamoja na ule wa “Kuongeza Uhimilivu wa Kijamii na Kiikolojia wa Mkondo wa Bahari ya Pemba Kupitia Usimamizi wa Jamii” unaotekelezwa na Shirika la Mwambao. Pia Shirika la WCS linatekeleza Mradi uitwayo “Bahari ni Urithi” utakaojikita katika kuimarisha usimamizi wa maeneo yetu ya kiikolojia ya matumbawe ya bahari dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na hususan katika mwambao wa mashariki wa kisiwa cha Pemba.

xiv. Katika Sekta ya Mafuta na Gesi, Serikali imefanya malipo ya fidia kwa wananchi walioathiriwa mali zao wakati wa zoezi la mtetemo, ambapo jumla ya wananchi 2,452 (1,638 kwa Unguja na 814 kwa Pemba) walilipwa kati ya wananchi 3,028 waliothibitishwa (verified) kulipwa. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 80.9 ya malengo yaliyowekwa. Jumla ya **Shilingi Milioni 947** zimelipwa kati ya **Shilingi Bilioni**

**1.3** zilizotengwa ambazo ni wastani wa **asilimia 87** ya fedha ambazo wananchi walioathirika na utafiti wa awali wa Mafuta na Gesi Asilia. Kiwango kidogo kwa wananchi wachache waliobakia watalipwa hivi karibuni.

xv. Katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, Kuandaa rasimu mbili za Kanuni za Udhibiti na Urejeshaji wa gharama za mkandarasi (Ring Fencing & Cost Recovery) na Kanuni ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibiliy) pamoja na kuandaa tafsiri za kanuni za tozo na vibali (Fee and Permit), Uchimbaji (Drilling) na Afya, Usalama na Mazingira (Health Safety and Environment) kwa lugha ya Kiswahili.

xvi. Kampuni ya ZPDC imefanikiwa kutowa mafunzo ya muda mrefu kwa Mfanyakazi mmoja (1) katika fani ya "Geology"; mafunzo kwa vitendo ya Utafutaji wa kina wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya mtetemo huko (3D seismic Survey) TPDC katika kitalu cha Ruvuma – Mtwara; mafunzo ya utafsiri wa Taarifa za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia, kuhudhuria Warsha ya Kampuni za Mafuta za Afrika, Johannesburg, South Africa. Aidha Kampuni imefanikiwa kuandaa "Business Plan" (Mpango wa Biashara) kwa mkondo wa chini hususan katika suala la uagizaji wa mafuta kwa wingi nchini (Bulk Procurement).

xvii. Kampuni ya ZPDC imetayarisha muongozo wa upokeaji, uhakiki na uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia, muongozo wa mafunzo (Training Guideline), na kupitiwa na Uongozi wa Kampuni. Halikadhalika Kampuni inaendelea na zoezi la kutafsiri Taarifa za Mafuta na Gesi.

xviii. Kampuni ya ZPDC imefanikiwa kutowa mafunzo ya muda mrefu kwa Wafanyakazi wawili (2) katika fani ya "Jiologia" na Fani ya Uchumi na Fedha, Kuingia mkataba wa mashirikiano (MoU) na Kampuni ya GEP kutoka Uingereza kwa jili ya kuandaa mkutano wa kimataifa wa Nishati na

Viwanda (Zanzibar Energy and Industrial Summit (ZEIS). Aidha, Kampuni imefanikiwa kuandaa ”Business Plan” (Mpango wa Biashara) kwa mkondo wa chini hususan katika suala la uagizaji wa mafuta kwa wingi nchini (Bulk Procurement).

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**22. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Programu zake kuu tatu (3) na Programu ndogo sita (6) ni kama ifuatavyo;

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**23. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Programu hii ina programu ndogo moja nayo ni Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na ina huduma mbili kama ifuatavyo:

i. Uratibu wa Uchumi wa Buluu
ii. Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu hii iliombewa **Shilingi 14,203,801,496.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,203,801,496** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 228,501,496** ni Mishahara, **Shilingi 1,200,000,000** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, na **Shilingi 1,775,300,000** ni Ruzuku kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA). Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 11,000,000,000**. Hadi kufikia Machi 2023, Programu hii imepata jumla ya **Shilingi 1,301,671,992** sawa na **asilimia 9** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo,

**Shilingi 95,686,680** ni kwa ajili ya matumizi ya Uendeshaji wa ofisi na **Shilingi 1,205,985,312** ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA). Hakuna fedha ya Miradi ya Maendeleo iliyopatikana kwa kipindi cha miezi tisa. **(Kiambatanisho Namb. 4)**

**Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu.**

**25. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla.

**26. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu ndogo hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Jumla ya programu 52 za uwelewa juu ya dhana ya uchumi wa Buluu zimefanyika.

ii. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kumi (10) kuhusu kuandaa mpango wa matumizi ya Bahari.

iii. Kuratibu na kuhudhuria majukwaa manane (8) yenye lengo la kukuza sekta ya uchumi wa buluu.

iv. Kufanyika kwa vikao kumi na saba (17) vya uandaaji wa mpango wa matumizi ya bahari.

v. Kuandaa kwa asilimia sitini (60) mfumo wa kupokea na kutunza Takwimu ya kazi za Uchumi wa Buluu (Dashboard).

**27. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu Ndogo hii iliombewa **Shilingi 1,428,501,496** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,200,000,000** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 228,501,496** ni Mishahara. Hadi kufikia Machi 2023, Programu hii imepata jumla ya **Shilingi 95,686,680** sawa na **asilimia 6.6** ya makadirio ya mwaka. **(Kiambatanisho Namb. 4)**

**Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA)**

28. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ni taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

29. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kupitia Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo;

    i. Mamlaka imeandaa Miongozo miwili (2) ya Kitaalamu kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya Mafuta na Gesi Asilia ambayo ni Kanuni ya Udhibiti na Urejeshaji wa gharama za mkandarasi (Ring Fencing & Cost Recovery) na Kanuni ya Uwajibikaji wa Makampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibility). Aidha, Mamlaka imefanikisha kazi ya kuandaa tafsiri za kanuni za tozo na vibali (Fee and Permit), Uchimbaji (Drilling) pamoja na kanuni ya Afya, Usalama na Mazingira (Health Safety and Environment) kwa lugha ya Kiswahili.

    ii. Mamlaka imefanikiwa kusimamia ulipaji wa fidia kwa Waathirika wa zoezi la Utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya Mtetemo (2D Seismic Survey) ambayo ni sehemu ya kazi ya kusimamia shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa kitalu cha Pemba – Zanzibar. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2023, jumla ya **Shilingi 900,000,000** zimelipwa kwa wananchi 2,452 (1,638 kwa Unguja na 814 kwa Pemba) kati ya wananchi 3,028 waliothibitishwa (verified) kulipwa fidia zao. Hii ni sawa na **asilimia 80.9** ya makadirio. Hata hivyo, kazi ya kufanya utafiti wa mtetemo wa kina (3D Seismic Survey) kwa kitalu cha Pemba – Zanzibar haikuweza kutekelezwa kama ilivyopangwa hadi kumalizika kwa muda aliopewa mkandarasi kimkataba. Aidha, mkandarasi ameiomba

kampuni ya ZPDC kulirejesha eneo lote la mkataba kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mujibu wa matakwa ya sheria na mkataba.

iii. Kwa upande wa mpango wa ugawaji wa vitalu vipya katika maeneo ya bahari ya mashariki ya visiwa vya Zanzibar, Mamlaka imefanikiwa kuingia mkataba na Kampuni ya Schlumberger kwa kazi ya Uchambuzi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia kwa lengo la kufungua maeneo mapya ya uwekezaji katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa upande wa baharini. Mpango wa ugawaji wa vitalu vipya unaotekelezwa na Kampuni hiyo umefikia asilimia sabini (70) ya malengo yake.

iv. Mamlaka imeendelea na kazi ya uimarishaji wa mfumo wa usimamizi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia, zikiwemo kukabidhiwa Data kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kampuni ya RAKGas, kuzifanyia uhakiki wa awali Data hizo pamoja na kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa kituo cha uhifadhi wa Data. Aidha, Mamlaka inaendelea na taratibu za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na ujenzi wa kituo cha muda cha kuhifadhia Taarifa (Temporary Data Centre) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Uanzishaji wa Kituo cha Taifa cha uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (National Data Repository - NDR).

v. Mamlaka imeendesha jumla ya programu 46 kati ya 60 zilizopangwa za kujenga uelewa kwa jamii kuhusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia.Programu hizi ziliendeshwa kupitia mikutano 14 ya taasisi, mikutano 17 ya wanashehia kwa Unguja na Pemba, kongamamano moja pamoja na programu 14 za vyombo vya habari kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC TV na ZBC Redio), TBC1 pamoja na magazeti ya Zanzibar Leo na Mwananchi.

vi. Kwa upande wa kuwajengea uwezo watendaji wa taasisi, Mamlaka imewezesha kuendesha mafunzo kumi na tatu ya muda mfupi (13) yakiwemo mafunzo ya vitendo. Aidha, mfanyakazi mmoja amefanikiwa kujiunga na mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya uzamivu kupitia ufadhili wa Serikali ya Norway.

**30.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) iliombewa jumla ya **Shilingi 6,775,300,000** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 602,100,000** ni Mishahara, **Shilingi 1,173,200,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 5,000,000,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023, Mamlaka imepatiwa jumla ya **Shilingi 1,205,981,312** kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 17.8** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 976,785,435** ni Mishahara na **Shilingi 229,195,877** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC)**.

**31.** **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar imelenga kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni.

**32.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kampuni tayari imeingia Mkataba wa Mashirikiano MoU na Kampuni ya GEP kutoka Uingereza kwa ajili ya kuandaa Mkutano wa kimataifa wa Mafuta na Gesi unaotegemewa kufanyika Julai 26 hadi 27 2023 katika Hoteli ya Golden Tulip, Jijini Zanzibar.

ii. Miongozo mitatu imendaliwa ambayo ni; Scheme of Service, Training Guideline na Store Guideline.

iii. Kuwalipia wafanyakazi wawili mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya kwanza katika fani ya Jiologia na Shahada ya uzamili katika fani ya Uchumi na Fedha

iv. Wafanyakazi wawili wanashiriki katika mafunzo ya muda mfupi kuhusiana na Sheria za Manunuzi na Uhusiano wa Habari.

v. Kutoa mafunzo ya ndani ya Udhibiti wa Viashiria Hatarishi (Risk Management) kwa Menejimenti ya Kampuni.

vi. Wafanyakazi 2 kuhudhuria mafunzo kwa vitendo ya Utafutaji wa kina wa mafuta na gesi asilia kwa njia ya mtetemo huko (3D seismic Survey) TPDC katika kitalu cha Ruvuma – Mtwara.

vii. Kutoa mafunzo ya utafsiri wa Taarifa za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa wataalamu 5 wa Mafuta na Gesi wa Kampuni.

viii. Wafanyakazi 6 kuhudhuria Kongamano la Nishati "Tanzania Energy Congress" huko Dar Es Salaam.

ix. Wafanyakazi 2 kuhudhuria Warsha ya Kampuni za Mafuta za Africa, Johannesburg South Africa.

x. Kushiriki kikao cha kujadili na kuunda kikosi kazi cha kupambana na umwagikaji wa mafuta pamoja na athari zake katika eneo la Baharini ya Tanzania.

xi. Kushiriki katika kikao cha mashirikiano baina ya TPDC na ZPDC katika afisi za TPDC Dar Es Salaam.

xii. Ulipaji wa leseni ya matumizi ya "Kingdom software".

xiii. Kufanya ukaguzi wa ndani wa Kampuni kwa Idara na Vitengo kwa kipindi cha miezi 12 kutoka Januari 2022 hadi Disemba 2022 na robo ya kwanza ya mwaka 2023

xiv. Kampuni iliweza kufanya vikao mbali mbali na wawekezaji wenye nia ya kuekeza katika Sekta ya Mafuta na Gesi kwa mkondo wa kati na wa chini ( Midstream and Downstream)

xv. Kampuni imefanikiwa kuandaa Mpango wa Biashara (Business Plan) kwa mkondo wa chini hususan katika suala la uagizaji wa mafuta kwa wingi nchini (Bulk Procurement).

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar iliombewa jumla ya **Shilingi 10,424,685,527** kwa matumizi ya kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,424,685,527** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 6,000,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo **(Kiambatanisho Namb. 2)**. Hadi kufikia Machi 2023, Kampuni ilipatiwa **Shilingi 1,344,949,492** sawa na **asilimia 12.9** ya makadirio ya mwaka. Ambapo **Shilingi 1,006,456,192** ni Mishahara na **Shilingi 338,493,300** kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI**

34. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni;

i. Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya baharini
ii. Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari

35. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu ya Maendeleo ya Uvuvi ni kuendeleza sekta ya Uvuvi na Mazao ya Baharini kwa kuongeza uzalishaji (fish catch) wa samaki na kuimarisha kilimo cha mwani, ufugaji wa viumbe maji na mazao mengine ya baharini. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 73,161,642,646**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,606,642,646** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,039,142,64**6 ni Mishahara, **Shilingi 935,000,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 632,500,000** ni

Ruzuku. Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 70,555,000,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 41,000,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 29,555,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

36. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi 2023, Programu hii ilipatiwa jumla ya **Shilingi 19,149,775,632** sawa na **asilimia 26** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,084,368,323** ni kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,398,323,744** ni Mishahara, **Shilingi 188,459,830** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 497,584,749** ni Ruzuku kutoka Serikalini (**Shilingi 130,104,750** kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini ZAFIRI na **Shilingi 367,479,999** kwa Kampuni ya Uvuvi ZAFICO). Kwa Miradi ya Maendeleo, Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 17,065,407,309** ambapo **Shilingi 2,070,000,000** kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na **Shilingi 14,995,407,309** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo **Shilingi 11,599,214,123** ni kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa mchango wa ujenzi wa Diko na Soko la kisasa Malindi ambao umekamilika, **Shilingi 3,016,019,434** ni kutoka Benki ya Dunia kwa mradi wa SWIOFISH ambao tayari umekamilika na **Shilingi 380,173,752** kutoka shirika la IFAD kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi **(Kiambatanisho Namb. 4)**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini**

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza Uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu ndogo hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Wizara imetoa taaluma ya Uvuvi kwa kamati 102 za Uvuvi unguja Na Pemba,

ii. Kutoa taaluma ya usarifu wa bidhaa za mwani kwa wajasiriamali mia moja (100),

iii. Mafunzo ya njia bora za kisasa za upandaji mwani yenye uwezo wa kuongeza uzalishaji wa mwani mara tatu hadi nne pamoja na utambuzi wa maeneo sahihi ya kuweka mashamba ya mwani yatakayosaidia kupunguza uwezekano wa mwani kushambuliwa na maradhi yametolewa kwa wakulima wa mwani wa Matemwe, Mwambale, Muyuni A, Kizimkazi, Ukongoroni, Kisakasaka, Bweleo, Fujoni, Kiongwe, Pongwe, Uzi, Kiongwe, Kidoti, Kiuyu Mbuyuni, Wingwi, Kisiwa Panza na Mjini Kiuyu.

iv. Jumla ya mashamba darasa 18 yameanzishwa katika vijiji 18 vya Unguja na Pemba. Vijiji hivyo ni Matemwe, Mwambale, Muyuni A, Kizimkazi, Ukongoroni, Kisakasaka, Bweleo, Fujoni, Kiongwe na Pongwe,Uzi, Kiongwe, Kidoti, Kiuyu Mbuyuni, Wingwi, Kisiwa Panza, Mjini Kiuyu

v. Majaribio ya kuzalisha mwani mnene (cottonii) yamefanyika kwa mafanikio katika eneo la Mwambale ambapo mwani unaozalishwa kutokana na majaribio hayo husambazwa kwa wakulima kama mbegu hapo kijijini na baadae kusambazwa kwenda vijiji vyengine ili kuongeza uzalishaji wa mwani mnene (Cottonii).

vi. Mafunzo ya siku sita juu ya utaratibu wa kusafirisha mazao ya baharini nje ya nchi pamoja na ukaguzi wa mazao hayo kabla ya kusafirishwa kuingia soko la china yametolewa na wakufunzi kutoka Tanzania Bara.

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **Shilingi 72,710,642,646.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,155,642,646** ni kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,039,142,646** Mishahara, **Shilingi 484,000,000** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 632,500,000** ni Ruzuku kutoka SMZ (**Shilingi 320,000,000** kwa Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini na **Shilingi 312,500,000** kwa Kampuni ya Uvuvi

ZAFICO). Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 70,555,000,000**. Kati ya hizo, **Shilingi 41,000,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 29,555,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

39. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2023, Programu ndogo hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 18,566,518,142** sawa na **asilimia 26** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,998,695,582** ni kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,398,323,744** ni Mshahara, **Shilingi 102,787,089** ni matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 497,584,749** ni Ruzuku kutoka Serikalini (**Shilingi 130,104,750** kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini ZAFIRI na **Shilingi 367,479,999** kwa Kampuni ya Uvuvi ZAFICO). Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 17,065,407,309** ambapo **Shilingi 2,070,000,000** ni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na **Shilingi 14,995,407,309** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo **Shilingi 11,599,214,123** ni kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa mchango wa ujenzi wa Diko na Soko la kisasa Malindi, **Shilingi 3,016,019,434** kutoka Benki ya Dunia kwa mradi wa SWIOFISH ambao tayari umekamilika na **Shilingi 380,173,752** kutoka shirika la IFAD kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya kilimo na Uvuvi **(Kiambatanisho Namb. 4)**.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini**

40. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini imetekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (ZAFIRI) imeingia makubaliano na Kampuni ya Afrivision katika uendeshaji wa kituo cha kutotolea vifaranga vya Samaki, kaa na Matango Bahari.

ii. Taasisi imefanikiwa kufanya utafiti wa vimelea katika Samaki kwa lengo la kumlinda mtumiaji na mlaji. Kwa sasa utafiti huu upo kwenye hatua za kukusanya sampuli za samaki katika maeneo ya madiko na masoko.

iii. Kufanya Utafiti juu ya hali halisi ya kimazingira katika hifadhi ya CHANGUU-BAWE (CHABAMCA) pamoja na kukusanya Taarifa za msingi.

iv. Taasisi imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi.

**41. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini iliombewa jumla ya **Shilingi 320,000,000** kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2023 Taasisi imepata jumla ya **Shilingi 130,104,750** sawa na **asilimia 41** ya fedha zilizopangwa.

**Kampuni ya Uvuvi Zanzibar – ZAFICO**

**42. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2022-2023, imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kampuni ya ZAFICO imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Biashara (2023-2028).

ii. Kuanza mafunzo ya uanikaji dagaa pamoja na uzalishaji kwa hatua za awali (majaribio).

iii. Kuweka miundombinu ya kuwezesha biashara ya samaki Pemba.

iv. Kuongeza wigo wa bidhaa za Samaki.

v. Kufanya tathmini ya kimazingira katika maeneo ya miradi ya Kampuni ikiwemo Fungurefu na Ndagoni.

vi. Kuingia makubaliano na Jeshi la Kujenga uchumi kwa ujenzi wa Kituo cha kisasa cha kuanikia madagaa huko Kama.

vii. Kuandaa jumla ya chanja 500 za kuanikia dagaa.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO iliombewa jumla ya **Shilingi 11,312,500,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 312,500,000** ni Ruzuku ya mishahara kutoka SMZ na **Shilingi 11,000,000,000** ni utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023, Kampuni imepatiwa jumla ya **Shilingi 367,479,999** kwa ajili ya Mishahara. Kampuni ya ZAFICO ilitarajia kupata **Shilingi 4.6** Bilioni ikiwa ni pato litokanalo na biashara zake za ndani. Hadi kufikia Machi Kampuni imepata jumla ya **Shilingi 59,145,165** ya fedha zilizopangwa. Aidha, kupitia Mradi wa Ahweni ya UVIKO19, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeipatia ZAFICO jumla ya **Shilingi 5,977,340,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa kilichopo Kama **(Kiambatanisho Namb. 5)**.

**Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari**

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuanza Utekelezaji wa Mradi wa Bahari ni Mali “Sustainable Blue Livelihood in Tanga Pemba Seascape” unaofadhiliwa na Serikali ya Ireland na unaotekelezwa na Shirika la IUCN.

ii. Kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Kijamii wa Maeneo ya Uhifadhi wa Bahari kupitia Mwambao

iii. Kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Bahari ni Urithi kupitia Shirika la WCS

iv. Utekelezaji wa Mradi wa Mashirikiano wa Nairobi Convention na FAO-SWIOFC kuhusiana na uvuvi endelevu unaojali uhifadhi wa bahari.

v. Utoaji wa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa watumiaji wa bahari wakiwemo wanafunzi ,wanajamii wavuvi,waendesha boti za kitalii, vijana na kinamama pamoja na kuandaa mtaala wa utoaji wa mafunzo ya upandaji wa matumbawe.

vi. Mafunzo ya kinadharia ya ufungaji wa maboya na kuyaweka katika eneo linalozunguka kisiwa cha Bawe na eneo la mwana wa mwana yamefanyika kwa lengo la kuweka mipaka ili kuimarisha udhibiti wa maeneo ya hifadhi.

**45. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu ndogo ya Uhifadhi iliombewa **Shilingi 451,000,000** kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2023, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 85,672,741** sawa na **asilimia 19** ya makadirio ya mwaka.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**46. Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kutoa huduma za kiofisi kwa ustawi na ufanisi wa sekta.

**Programu imegawika katika programu ndogo tatu nazo ni:**

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji
ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti
iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba.

**47. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliombewa jumla ya **Shilingi 2,296,955,858** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,162,155,858** ni Mishahara, na **Shilingi 1,134,800,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2023, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 1,591,569,160** sawa na **asilimia 69** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,174,952,839** ni Mishahara na **Shilingi 416,616,321** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

   i. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 221
   ii. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 8 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na 41 mafunzo ya muda mfupi.
   iii. Ufuatiliaji na udhibiti wa Mali za Serikali.
   iv. Kutengeneza Mpango wa Rasilimali watu, Mpango wa Mafunzo, Mpango wa Urithishaji madaraka na Mpango wa manunuzi ya Wizara.
   v. Kutengeneza Tovuti ya Wizara.
   vi. Kutengeneza Mkataba wa Huduma kwa Wateja, Mkataba wa majukumu pamoja na Upimaji wa Utendaji wa Wafanyakazi.
   vii. Kuendelea kutoa taarifa za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia vyombo vya habari, majarida na njia ya mtandao na kuandaa vipindi vya TV na redio.

50. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, iliombewa jumla ya **Shilingi 1,025,448,539** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 450,448,539** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 575,000,000** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2023 Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 719,977,332** sawa na **asilimia 70** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 441,830,005** ni Mishahara na **Shilingi 278,147,327** ni kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kukamilisha Sheria ya Uvuvi, Sheria ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari na Sheria ya Uhifadhi na kuwasilisha katika vikao vya Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi.

ii. Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji na usambazaji wa takwimu.

iii. Kushirikiana na Tume ya Mipango katika Kuandaa miradi 17 mipya ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na kuratibu usimamizi wa miradi inayoendelea ya Wizara (**Kiambatanisho Namb. 9**).

iv. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti na mpango kazi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na kuwasilisha utekelezaji kwa mujibu wa miongozo ya Baraza la Wawakilishi na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

v. Kuratibu kazi za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vi. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa kazi za Wizara na miradi ya maendeleo.

vii. Kusimamia na kuratibu uandaaji wa Hati tisa (9) za mashirikiano kuhusu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi baina ya Wizara na Taasisi zake pamoja na Kampuni mbali mbali.

viii. Kuratibu Mashirikiano ya Wizara za SMT na SMZ pamoja na mashirikiano ya ndani, kikanda na kimataifa.

53. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango kwa mwaka 2023 iliombewa jumla ya **Shilingi 574,317,420** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 134,517,420** ni Mishahara, na **Shilingi 439,800,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufika Machi 2023, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 238,489,309** kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 42** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 134,046,194** ni Mishahara na **Shilingi 104,443,115** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba**

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kushiriki katika maadhimisho mbali mbali ya kitaifa ikiwemo kupinga ukatili na udhalilishaji wa wanawake.

ii. Kuratibu ziara nane (8) za viongozi wa Wizara na Kitaifa.

iii. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, na taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

iv. Jumla ya vikao 4 vimefanyika ikiwemo kuanzishwa bandari za uvuvi, kujadili rasimu ya kanuni za uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, mkutano wa kujadili maendeleo ya soko la Tumbe na ukusanyaji wa mapato, na kikao cha kupitia

rasimu wa mkataba wa mgawanyo wa mapato ya uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

v. Kufanyika kwa vikao mbali mbali vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na Idara na taasisi mbali mbali mtambuka za Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

**56.** **Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 697,189,899** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 577,189,899** ni Mishahara na **Shilingi 120,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2023, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 633,102,516** sawa na **asilimia 91** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 599,076,640** ni Mishahara na **Shilingi 34,025,879** kwa matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## CHANGAMOTO

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitahada za Wizara na Serikali kwa ujumla, Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na:

| | CHANGAMOTO | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| 1) | Kuchelewa kuanza utekelezaji wa Miradi mikubwa ya maendeleo kutokana na uchelewaji wa kuidhinishwa na washirika wa maendeleo. | Wizara imeendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuhakikisha kuwa changamoto zote zinazochelewesha kuanza kwa miradi hiyo zinasuluhishwa kwa uharaka. |
| 2) | Kukwama au kushindwa kuanza kwa baadhi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa kupitia ubia na wawekezaji kwa sababu za kifedha | Wizara imeendelea kutafuta vyanzo vyengine vipya vya mbali mbali vya miradi ya ubia na Sekta binafsi, ikiwemo kumaliza na kufuta mikataba yote inayokwamisha juhudi za Serikali za kuwaletea maendeleo wananchi wake. |
| 3) | Uhaba wa wataalamu kwenye sekta ya Mafuta na Gesi Asilia | Wizara inaendelea kusomesha na kuajiri watendaji wenye sifa. |
| 4) | Uhaba wa teknolojia, nyenzo na wataalamu wa kufanya tafiti bora za uvuvi na mazao ya bahari. | Wizara inaendelea kuajiri watendaji wenye sifa pamoja na kununua vifaa na pia kuingia katika mashirikiano na wadau mbali mbali wa Sekta hii. |

| | | |
|---|---|---|
| 5) | Ukosefu wa Wataalamu wa Uvuvi wa Bahari Kuu kwa Kampuni ya ZAFICO. | Wizara inaendelea na utaratibu wa kutafuta wavuvi wenye uzoefu wa kazi za uvuvi ikiwemo kutumia njia endelevu za mashirikiano na ubia katika sekta binafsi. |
| 6) | Kuendelea kwa uharibifu wa mazingira ya bahari, uvuvi haramu katika maeneo ya Bahari. | Wizara inaendelea na programu zake za ushajiishaji kwa jamii na pia ipo katika michakato ya kukamilisha miongozo na Sheria mpya za Sekta ya Uvuvi na uhifadhi wa bahari. |

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024MAKADIRIO YA MAPATO 2023/2024**

**58. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 5,727,275,000** kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Namb. 7**).

**MAKADIRIO YA MATUMIZI 2023/2024**

**59. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 Wizara inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 81,061,012,171**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 9,313,000,000** ni kwa kazi za kawaida na **Shilingi 71,748,012,171** ni kwa kazi za maendeleo. **(Kiambatanisho Namb. 8)**

**60. Mheshimiwa Spika,** Mgawanyiko wa fedha za kawaida ni **Shilingi 9,313,000,000**. Kati ya hizo, Shilingi 3,814,300,000 ni Mishahara, **Shilingi 2,452,400,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa ofisi na **Shilingi 3,046,300,000** ni Ruzuku kutoka SMZ. Kwa fedha za Ruzuku, **Shilingi 240,000,000** ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini, **Shilingi 1,498,300,000** ni kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, na **Shilingi 428,100,000** ni kwa ajili ya Kampuni ya ZAFICO. **(Kiambatanisho Namb. 8)**.

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Wizara inaombewa jumla ya **Shilingi 71,748,012,171**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 35,500,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 36,248,012,171** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambapo **Shilingi 19,421,033,471** ni Mkopo na **Shilingi 16,826,978,700** ni Ruzuku (**Kiambatanisho Namb. 8**). Aidha, Jumla ya **Shilingi 2.5 Bilioni** zimetengwa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA

62. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 itatekeleza malengo yake kupitia Programu zake kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;
ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo yenye thamani ya **Shilingi 71,748,012,171** kama ifuatayo:

i. Mradi wa kuendeleza Kilimo na Uvuvi unaofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo – IFAD. (Agriculture and Fisheries Development Programme - AFDP).

ii. Mradi wa Uimarishaji wa Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia - TASFAM (Tanzania Scaling Up Sustainable Fisheries and Aquaculture Management Project).

iii. Mradi Jumuishi wa Kuhifadhi Ikolojia na Kuendeleza Uchumi wa Bahari Tanzania (Leading an ecological and inclusive Ocean Base Economic Growth in Tanzania) unaofadhiliwa kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Ufaransa (AFD).

iv. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha kuhifadhia Gesi Asilia na Mindombinu ya Usambazaji wa Gesi.

v. Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Kuhifadhia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia.

vi. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli iliyosafishwa na Usambazaji (Bulk Storage Facility).

vii. Ujenzi wa Diko na Soko la kisasa katika eneo la Kama - Unguja (Construction of Fish Landing Site and Market Facilities).

viii. Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Mangapwani (Construction of Fish Port).

ix. Mradi wa kuboresha miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za baharini.

x. Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini (Women Empowerment in Integrated Mariculture Value Chain in Zanzibar) unaofadhiliwa na Shirika la KOICA.

xi. Mradi wa "Bahari Maisha" kwa lengo la Kuendeleza Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Bahari unaofadhiliwa na UNDP.

xii. Mradi wa Uchumi wa Buluu kwa Kutengeneza Ajira na Kukabiliana Mabadiliko ya Tabia Nchi (Blue Economy for Job Creation and Cimate Change Adaptation) unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (European Union).

xiii. Mradi wa Mashirikiano wa Masuala ya Bahari na Uongozi wa Uvuvi kwa Nchi za Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SwioFC Nairobi Convention Partnership Project) wenye lengo la Kuboresha shughuli mbadala za jamii katika ukanda wa Pwani unaofadhiliwa na Shirika la FAO.

xiv. Mradi wa Utafiti wenye lengo la Kudumisha Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii unaofadhiliwa na Shirika la NORAD (Fisheries Livelihood and Governance Project SAMAKI)

xv. Mradi wa Tafiti wa "Zan Blue Project" unaofadhiliwa na FINLAND.

xvi. Mradi wa Kuboresha Mifumo ya Ukusanyaji wa Tozo katika maeneo ya Hifadhi unaofadhiliwa na Shirika la UNDP (Biofin Project).

**64. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar – ZAFICO imepanga kutekeleza miradi ya ubia na makampuni ya ndani na nje ya nchi kama ifuatayo;

i. Mradi wa uwekaji wa Mitambo ya Kuhifadhi Baridi (Pilot Implementation and Development of Zero Energy Seafood chain) unaofadhiliwa na Shirika la KOICA.

ii. Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Ndagoni wenye thamani ya **Shilingi Bilioni 10**.

iii. Mradi wa ufugaji wa samaki kwa njia za matenga, Bwereu –Kidoti wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 10.

iv. Mradi jumuishi wa uvuvi na usarifu wa mazao ikiwemo uwekaji wa mitambo ya baridi na uzalishaji wa samaki. Mradi huu ni mashirikiano na Senegal na Marekani.

v. Kuendelea na Ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Kama kupitia programu ya UVIKO 19 na mikopo ya Benki.

**65. Mheshimiwa Spika, Aidha**; Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 itatekeleza jumla ya miradi mengine mitano (5) kwa mashirikiano na Taasisi zisizo za Serikali (NGO's) kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Heshimu Bahari unaofadhiliwa na USAID wenye thamani ya Dola za Kimarekani **US$ 13 Milioni.**

ii. Mradi wa Bahari Mali unaofadhiliwa na Ubalozi wa Jamhuri ya Ireland wenye thamani ya **Euro 1.8 Milioni**.

iii. Mradi wa Bahari ni Urithi unaotekelezwa na Shirika la WCS kupitia mfuko wa "Blue Action Fund" wenye thamani ya **Euro 5.8 Milioni**

iv. Mradi wa Usimamizi wa Kijamii wa Maeneo ya Kiikolojia ya Bahari unaotekelezwa na Shirika la Mwambao kupitia "Blue Action Fund". Mradi huu unagharimu **Euro 6.4 Milioni**.

v. Mradi wa Miamba Yetu unaofadhiliwa na "Global Fund for Coral Reefs" wenye thamani ya **US$ 2 Milioni**.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi itaendelea na uwezeshaji wa jamii kwenye miradi ya kuleta Ahueni ya UVIKO 19. Aidha, pamoja na miradi hiyo, Wizara itashajihisha jamii kupitia Programu ya uwezeshaji ya wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi "Blue Economy Intervention Plan".

## MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2023/2024

67. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni Kukuza Uchumi wa Zanzibar kwa kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za kisasa, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya uwekezaji na uimarishaji wa minyororo ya thamani (miundombinu na huduma) ambayo itasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana kupitia Uchumi wa Buluu.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo; Elimu na uwezeshaji, Usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari, Utafiti wa uvuvi na maliasili za bahari,

Ujenzi wa miundombinu (Bandari, Madiko, Masoko na Usarifu), Kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya baharini na kuhakikisha upatikanaji wa Rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia.

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeweka malengo ya usimamizi endelevu wa Bahari katika kuimarisha maendeleo ya Uchumi wa Buluu Zanzibar kama ifuatavyo;

i. Kuendelea na taratibu za ununuzi wa Meli moja kubwa ya kisasa ya Uvuvi.

ii. Kuanza hatua za awali za mchakato wa upembuzi yakinifu kuelekea ujenzi wa bandari ya Uvuvi katika eneo la Mangapwani Unguja

iii. Kuendelea na Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Usarifu wa Dagaa ikiwemo ujenzi wa Diko na Soko la Samaki katika eneo la Kama Unguja

iv. Ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu samaki Fungurefu na mitambo ya baridi kupitia kampuni ya ZAFICO.

v. Kuendelea na matayarisho na utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya baharí (Marine Spatial Plan).

vi. Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini na ukulima wa mwani kibiashara.

vii. Kukamilisha Upokeaji na Ugawaji kwa wananchi **boti 1077** za Uvuvi na Ukulima wa Mwani pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau wa Sekta ya Uchumi wa Buluu wakiwemo wafaidika wa fedha za ahweni ya UVIKO19.

viii. Kuongeza shabaha ya utoaji wa leseni na vibali kwa meli za uvuvi wa bahari kuu.

ix. Kuwasilisha Sheria ya Uvuvi, Sheria ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari na Sheria ya Uhifadhi wa Bahari katika Baraza la Wawakilishi.

x. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa Bohari ya Mafuta (Bulk Storage facilities) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa mafuta.

xi. Kuanza hatua za awali za Ujenzi wa Bohari ya Gesi (Natural Gas/LPG Storage Facility) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa Gesi.

xii. Kuanza hatua za awali za kituo cha kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (National Data Repository au NDR)

xiii. Ujenzi wa maabara moja (1) kwa ajili ya utoaji wa mbegu bora za mwani kupitia mfumo wa "Tissue Culture".

xiv. Kuanza Ujenzi wa Vituo viwili (Unguja 1 na Pemba 1) vya utoaji wa mafunzo ya Uvuvi na ufugaji wa Mazao ya Baharini

xv. Kufungua maeneo mapya kwa ajili ya kuwaalika wawekezaji waendelee na utafiti wa uendelezaji wa utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU**

**70.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu imegawika katika programu ndogo moja nayo ni programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Aidha, Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ina huduma zake kuu mbili ambazo ni Uratibu wa Uchumi wa Buluu na Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

**71.** **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi 17,147,383,200**. Kati ya hizo **Shilingi 167,083,200** ni Mishahara, **Shilingi 602,100,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi

na **Shilingi 2,378,200,000** ni Ruzuku kwa ZPRA. Matumizi ya fedha za Ruzuku za ZPRA ni kama ifuatavyo: **Shilingi 1,498,300,000** ni Mishahara na **Shilingi 879,900,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa ofisi. Aidha Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imepangiwa kutumia **Shilingi 14,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu**

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Uchumi wa Buluu kupitia huduma zake inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kufanya utafiti wa utambuzi wa hali halisi ya matumizi ya maeneo ya bahari;
ii. Kufanya uchambuzi wa kisera na muundo utakaosaidia Mpango wa matumizi ya maeneo ya bahari;
iii. Kushajiisha shughuli za uratibu miongoni mwa sekta za kipaumbele za Uchumi wa Buluu;
iv. Kuhamasisha na kujenga uwezo kwa jamii kuhusu Uchumi wa Buluu;
v. Kuratibu uwezeshaji, uongezaji thamani na kuimarisha masoko ya bidhaa za Uchumi wa Buluu;
vi. Kuratibu utambuzi wa mahitaji katika kuandaa na kusimamia ‘Dashboard’ ya Uchumi wa Buluu na ‘Akaunti ya Satellite’; na
vii. Kuratibu ushiriki wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika shughuli za Uchumi wa Buluu.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **Shilingi 17,147,383,200**. Kati ya hizo **Shilingi 167,083,200** ni Mishahara, **Shilingi 602,100,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi

na **Shilingi 2,378,200,000** ni Ruzuku kwa ZPRA. Matumizi ya fedha za Ruzuku za ZPRA ni kama ifuatavyo: **Shilingi 1,498,300,000** ni Mishahara na **Shilingi 879,900,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi. Aidha, Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imepangiwa kutumia **Shilingi 14,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,000,000,000** ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bahari Maisha na **Shilingi 8,000,000,000** ni kwa ajili ya Programu ya Mafuta na Gesi Asilia.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA)**

**75. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inalenga kuendeleza majukumu yake ya kusimamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia imepanga kutekeleza Majukumu yake kupitia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kukamilisha kazi ya ugawaji wa vitalu vipya vya utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Maeneo ya upande wa mashariki ya bahari ya Zanzibar kupitia mkataba ulioingiwa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kampuni ya Schlumberger.

ii. Kuvitangaza vitalu vipya vya Zanzibar katika majukwaa mbali mbali kwa wawekezaji wa sekta ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

iii. Kuendeleza mazungumzo na wawekezaji waliopo na watakaojitokeza wenye nia ya kuwekeza nchini katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

iv. Kukamilisha zoezi la ulipaji fidia kwa waathirika wa zoezi la utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya mtetemo lililofanywa na Kampuni ya RAKGas.

v. Kuendeleza kazi za uimarishaji wa mfumo wa usimamizi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kutoa taarifa na machapisho kuhusiana na shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

vi. Kufanya mapitio ya Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia nambari 6 ya mwaka 2016 pamoja na kuandaa miongozo minne (4) ya udhibiti wa sekta ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

vii. Kuendelea kushirikiana na Wadau mbali mbali wa sekta wakiwemo washirika wa Maendeleo katika kuimarisha mashirikiano ya sekta kwa lengo la kutekeleza kazi na mipango ya mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia kwa watendaji wa Mamlaka.

viii. Kuendesha Programu za kutoa uelewa kwa jamii kuhusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ambapo jumla ya programu 54 zitaendeshwa kupitia mikutano ya taasisi, vyombo vya habari, makongamano pamoja na mikutano ya wanashehia za Unguja na Pemba.

ix. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa watendaji ikiwemo ubora wa Ofisi, nguvu kazi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi waliopo ili kuleta ufanisi zaidi kwa Mamlaka.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inaombewa jumla ya **Shilingi 6,378,200,000**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,498,300,000** ni Mishahara na **Shilingi 879,900,000** ni matumizi ya uendeshaji wa ofisi na **Shilingi 4,000,000,0000** ni kwa kutekeleza mradi wa maendeleo.

**Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, ZPDC**

78. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inalenga kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Ujenzi wa Bohari ya Kuhifadhia Mafuta ikiwa ni hatua za awali za ununuzi na uhifadhi wa Mafuta kwa jumla.

ii. Ujenzi wa kituo cha kuhifadhia Gesi Asilia na miundombinu ya usambazaji.

iii. Kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi kwa Wafanyakazi.

iv. Kujenga uwezo kwa Watendaji wa Kampuni katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia;

v. Uendeshaji wa shughuli za Mkataba wa mgawanyo wa Mafuta na Gesi Asilia (PSA);

vi. Ununuzi wa vifaa vya kuhifadhia Taarifa za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa Majiolojia pamoja na kuanzisha mfumo wa akiba wa kuhifadhi Taarifa za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia;

vii. Kutoa uelewa wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi za Serikali na wananchi.

viii. Kushiriki katika biashara ya Mafuta na Gesi kwa mkondo wa kati na chini kupitia Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

80. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inaombewa jumla ya **Shilingi 6,500,000,000**. Kati ya hizo **Shilingi 2,500,000,000** kwa ajili ya uendeshaji wa Kampuni na S**hilingi 4,000,000,000** kwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

81. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari;

**82. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi 57,513,841,671**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 3,265,829,500** ni kwa matumizi ya kawaida ambapo, **Shilingi 1,886,533,500** ni Mishahara, **Shilingi 711,196,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa ofisi, na S**hilingi 668,100,000** ni Ruzuku. Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi 54,248,012,171**. Kati ya hizo **Shilingi 27,500,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 26,748,012,171** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini**

**83. Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu ndogo hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza taratibu za ununuzi wa meli za kisasa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu.

ii. Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu samaki katika eneo la Fungurefu - Mkokotoni.

iii. Ujenzi wa mitambo ya baridi kupitia mfumo wa umeme wa jua.

iv. Kuendelea kuimarisha kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji wa mwani kutoka **tani 12,594** hadi **tani 15,000** kwa kuwapatia elimu ya kisasa ya ukulima wa mwani pamoja na vifaa vitakavyosaidia kuongeza uzalishaji.

v. Kukamilisha upokeaji na ugawaji wa **boti 1077** za uvuvi na ukulima wa mwani.

vi. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa diko na soko la kisasa katika eneo la Kama-Unguja.

vii. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa Bandari ya uvuvi katika eneo la Mangapwani - Unguja.

viii. Kuendelea kutoa elimu ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini kwa vikundi 350 Unguja na Pemba.

**84. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **Shilingi 47,575,426,971**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,254,393,500** kwa matumizi ya kawaida, ambapo **Shilingi 1,886,533,500** ni Mishahara na **Shilingi 367,860,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji ya ofisi. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi 45,321,033,471**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 23,500,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 21,821,033,471** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini**

**85. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kufanya tafiti mbili zinazohusiana na sekta ya uvuvi na kutoa taarifa za utafiti huo

ii. Kutoa mafunzo kuhusu matokeo ya taarifa za utafiti

iii. Kutoa miongozo minne (4) ya kuendeleza utafiti

iv. Kuanzisha maabara ya “tissue culture” kwa uzalishaji wa mbegu bora za mwani.

v. Kushirikiana na Kampuni ya Afrivision katika utekelezaji wa programu ya uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari, kaa na samaki kupitia Kampuni ya Zanzibar Hatchery Ltd.

**86. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inaombewa jumla ya **Shilingi 5,014,832,528**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 240,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 4,774,832,528** ni kwa utekelezaji wa kazi za Maendeleo ambapo **Shilingi 4,000,000,000** kutoka SMZ na **Shilingi 774,832,528** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Kampuni ya Uvuvi Zanzibar ZAFICO***

**87. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) kwa mwaka wa fedha 2023/2024, inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Kama.

ii. Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kusarifu samaki Fungurefu-Mkokotoni

iii. Kushirikiana na sekta binafsi katika kundeleza uvuvi na ufugaji wa kisasa wa mazao ya baharini (samaki, kamba).

iv. Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 1,000 kwa ajili ya kuongeza thamani na ubora wa dagaa wa Zanzibar

v. Kuendelea na matayarisho ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Samaki Shumba Mjini kwa upande wa Pemba

vi. Kuendeleza Mradi wa Uuzaji wa Samaki

vii. Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa samaki wa matenga wa Kampuni ya Zanzibar Aquaculture Harvest Company (ZAHC).

viii. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa kituo cha kusarifu dagaa Ndagoni - Pemba

**88. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO imeombewa jumla ya **Shilingi 964,846,172.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 428,100,000** ni Ruzuku ya mishahara kutoka SMZ na **Shilingi 536,746,172**

kwa utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo (Pilot Implementation and Development of Zero Energy Seafood Cold Chain). Aidha, Kampuni ya ZAFICO inategemea kutekeleza jumla ya miradi mitano ya Ubia na kampuni za ndani na nje ya nchi yenye wastani wa **Shilingi Bilioni 40**.

**Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari**

**89. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kutoa elimu ya Uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 102 Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufungaji wa pweza na samaki wa miambani.

ii. Kuanzisha mifumo ya kieletroniki ya ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya hifadhi.

iii. Kuimarisha Doria shirikishi 340 katika maeneo ya Maji ya Ndani kwa kununua **boti 5** za Doria ili kudhibiti Uvuvi haramu.

iv. Kuwawezesha jamii kuweka matumbawe Bandia katika maeneo saba ya Hifadhi za bahari ili kuongeza uzalishaji wa samaki.

v. Kuongeza maeneo mapya ya hifadhi shirikishi.

vi. Kufanya ufuatiliaji katika maeneo ya miamba na mazalia ya samaki.

vii. Kufanya usafi wa fukwe na mafungu.

viii. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi kumi kuhusu usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari.

ix. Kufanya kazi na sekta binafsi pamoja na washirika wa maendeleo katika kuendeleza uhifadhi wa mazingira ya bahari.

90. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu hii ndogo ya Uhifadhi inaombewa jumla ya **Shilingi 3,958,736,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 343,336,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 3,615,400,000** ni kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

91. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi lengo lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ustawi na ufanisi wa sekta.

**Programu imegawika katika programuu ndogo tatu nazo ni:**

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji
ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti
iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba

92. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inaombewa jumla ya **Shilingi 6,399,787,300** kati ya fedha hizo **Shilingi 2,899,787,300** ni kwa matumizi ya kawaida ambapo **Shilingi 1,760,683,300** ni Mishahara, **Shilingi 1,139,104,000** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 3,500,000,000** ni kwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

93. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kutoa stahiki kwa wafanyakazi 221.

ii. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 221, kwa mafunzo ya muda mrefu 8 na mafunzo ya muda mfupi 36 na mafunzo ya ndani 221

iii. Kutoa mikataba ya makubaliano ya majukumu kwa wafanyakazi 221.

iv. Kupima utendaji wa majukumu kwa wafanyakazi 221.

v. Ufuatiliaji na udhibiti wa Mali za Serikali.

vi. Kukamilisha Hifadhi Data ya Rasilimali Watu (Human Resource Data Base) pamoja na Tovuti ya Wizara.

vii. Kutengeneza Mkataba wa Huduma kwa Wateja pamoja na Kutekeleza Upimaji wa Utendaji wa Wafanyakazi.

viii. Kutoa taarifa za Wizara kupitia vyombo vya habari, majarida na njia za mtandao na Kuandaa vipindi vya TV na redio.

**94. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, inaombewa jumla ya **Shilingi 1,430,039,380** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 829,843,380** ni Mishahara na **Shilingi 600,196,000** ni kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

**Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

**95. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kuwasilisha Sheria tatu (3) za Wizara (Sheria ya Uvuvi; Uhifadhi wa Bahari na Utafiti wa Maliasili za Bahari katika vikao vya Baraza la Wawakilishi.

ii. Kufanya tafiti mbili (2) za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa agenda ya Utafiti ya Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo.

iii. Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji na usambazaji wa Takwimu.

iv. Kushirikiana na Tume ya Mipango katika Kuandaa na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi pamoja na kusimamia jumla ya miradi 17 ya Wizara itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

v. Kuandaa Mpango kazi, Bajeti ya Wizara na Ripoti za utekelezaji kwa kila robo mwaka.

vi. Utekelezaji wa kazi za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vii. Kutekeleza Mradi Jumuishi wa kuhifadhi Ikolojia na kuendeleza Uchumi wa Bahari Tanzania.

viii. Kuratibu vikao vya Mashirikiano ya Wizara kwa SMT na SMZ pamoja na mashirikiano ya ndani, kikanda na kimataifa.

**96. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango inaombewa jumla ya **Shilingi 3,872,045,660**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 112,045,660** ni Mishahara, na **Shilingi 260,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo programu hii imeombewa jumla ya **Shilingi 3,500,000,000.**

**Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba**

**97. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**98. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu vikao 4 na ziara za Kamati ya Uchumi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara Pemba.

ii. Kufanikisha ziara 10 za viongozi wa Wizara na Kitaifa.

iii. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, na taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

iv. Kufanya vikao vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na Idara na Taasisi mbali mbali mtambuka za Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

v. Kuimarisha mashirikiano na Taasisi nyenginezo za Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii.

**99. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi 1,097,702,260** ni kwa matumizi ya kawaida , Kati ya fedha hizo **Shilingi 818,794,260** ni Mishahara na **Shilingi 278,908,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Ofisi.

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

**100. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 5,727,275,000** kupitia vianzio vyake vinne vya Unguja na Pemba.

**101. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 81,061,012,171**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 9,313,000,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo **Shilingi 3,814,300,000** Mishahara, **Shilingi 2,452,400,000** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa

Ofisi na **Shilingi 3,046,300,000** ni Ruzuku kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar. Kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Wizara imetengewa **Shilingi 71,748,012,171**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 35,500,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 36,248,012,171** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ambapo **Shilingi 19,421,033,471** ni Mkopo na **Shilingi 16,826,978,700** ni Ruzuku.

## HITIMISHO

**102. Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa nachukua nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika utekelezaji wa programu na utoaji huduma za Uchumi wa Buluu ikiwemo sekta za Uvuvi, Ukulima wa Mwani, Ufugaji wa Mazao ya Baharini, Utafiti,Uhifadhi wa Bahari, na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais (Ikulu); Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao wamekuwa karibu sana nasi katika kulipeleka mbele gurudumu letu la maendeleo ya Uchumi wa Buluu; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ikiwemo pia wadau wetu wa karibu kabisa wa Uchumi wa Buluu ambao ni KMKM; Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ikiwemo ZIPA; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

